Jason E. Dunford

Intermediate Swahili

26 Feb 2006

Jiji la Zanzibar

Jiji la Zanzibar ni Mji Mkuu katika kisiwa cha Unguja ambacho, pamoja na kisiwa cha Pemba na visiwa vidogovidogo vingine kwa mfano Mnemba, ni funguvisiwa la Jamhuri ya Watu wa Zanzibar. Jamhuri hii ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Ramani ya Kisiwa cha Unguja ionyeshayo Jiji la Zanzibar (courtesy University of Texas)

Kisiwa cha Unguja kiko katika Bahari Hindi na ni takribani kilomita arobaini kutoka bara ya Tanzania. Jiji la Zanzibar liko katika pwani ya magharibi ya kisiwa hiki, katika mkoa wa Unguja Mjini Magharabi ambao ni kati ya mikoa ishirini na sita ya Tanzania. Kisiwa cha Unguja kina eneo la takribani kilomita mraba 1,658 na kina wakazi 460,000 (kati ya wakazi takriban 981,754 katika Jamhuri ya Watu wa Zanzibar yote) ambao takribani 207,000 wanaishi jijini Zanzibar[1].

Historia[2]

[1] Takwimu kutoka sensa ya mwaka elfu 2002, http://www.tanzania.go.tz/census/

Wakazi wa kwanza kisiwani Unguja walifika kutoka bara ya Afrika mnamo karne ya kumi na moja. Walikuwa wanachama wa makabila mbalimbali, kwa hivyo walipofika Unguja waliishi katika vijiji vidogovidogo bila serikali ya kati. Aidha, Waarabu walianza kufika Unguja katika nyakati hizi na msikiti wao unatoa tarehe thabiti ya kwanza ya watu kuishi Unguja: mwaka wa 1107. Lakini msikiti huo maalum uko katika kijiji cha Kizimkazi kuelekea kusini ya kisiwa, na tunadhani Waarabu hawakujenga kwa ardhi ambayo leo ni mahali pa Jiji la Zanzibar. Waarabu walipendelea kukaa hapo Kizimkazi na pia katika Unguja Ukuu, ambapo walijenga makazi yao. Watu wa kwanza ambao walifika Zanzibar na walianza kujenga kwa ardhi ya Jiji la Zanzibar ya leo, walikuwa Wareno.

Mnamo mwaka wa 1500, baada ya mvumbuzi maarufu, Vasco da Gama, kufika Afrika Mashariki, Wareno walifukuza Waarabu kutoka kisiwa cha Unguja. Walitaka kuongeza Unguja kwa makoloni ya Ureno, ili majahazi yao yaweze kulalapo kwa siku chache, kabla ya kuvuka Bahari ya Hindi kwenda nchi ya Uhindi. Huko nchini Uhindi, Wareno walikuwa na koloni lingine lililoitwa Goa. Wareno walichagua kisiwa cha Unguja, kama mahali pa kujenga mji na bandari, kwa sababu ya maji safi, rutuba ya ardhi na wanyama wakali wengi ambao wangeweza kutumia kwa chakula katika safari za majahazi yao. Aidha, kwa sababu Unguja ni kisiwa, Wareno wangeweza kukikinga kwa urahisi zaidi. Mji wao uliitwa Mji wa Mawe (maana yake katika Kiingereza ni *'Stonetown'*) na leo ni kitovu cha historia katika Jiji la Zanzibar. Wareno walikaa Unguja mpaka mwaka wa 1698, Waarabu waliporudi kuwatoa na kutawala Unguja tena. Waarabu hao, ambao walitoka nchini Oman, walipata kulipiza kisasi chao.

Katika utawala wa pili wa Waarabu ambao ulidumu hadi mwaka wa 1890, waliongeza majengo mengi katika Mji wa Mawe. Ili waweze kukinga kisiwa chao, walijenga ngome kubwa,

---

[2] Mambo kutoka http://www.africatravelresource.com/africa/E/zanzibar/accommodation/00.htm#

ambayo leo inaitwa *Ngome Kongwe*, na watu walijenga nyumba zao karibu na ngome hii. Maendeleo ya kwanza yalikuwa polepole, na hakukuwa na majengo mengine yo yote ya ukubwa ambayo yalijengwa mpaka karne ya kumi na tisa. Katika karne hii vitu vilikuwa vikibadilika Kisiwani Unguja, hasa katika Mji wa Mawe.

Kiongozi wa Waarabu, ambaye aliitwa Said bin Sultan, aliamua kuuhamisha Mji Mkuu wa Oman kutoka Muscat na kuuweka Mji wa Mawe. Kwa sababu ya uamuzi huu, saizi ya Mji wa Mawe ilianza kuongezeka zaidi. Wananchi wengi wa Oman walivutwa kwenda Unguja na hadithi kuhusu mali ambayo mtu anaweza kuipata huku kisiwani. Walikuja wakitarajia kuchuuza pembe na watumwa au kuwa wakulima wa karafuu na viungo. Waarabu wengi walifaulu katika biashara zao, na walitumia faida hizi kujenga nyumba kubwa ambapo wangeweza kuishi pamoja na familia zao. Hata leo nyumba nyingi kutoka kipindi hicho bado zinasimama na ni maarufu katika Afrika Mashariki kwa sababu ya milango yao, ambayo ilichongwa vizuri.

Lakini kwa sababu ya biashara ya watumwa, Jiji la Zanzibar lilianza kupata sifa mbaya kote duniani hasa katika Uingereza. Said bin Sultan alikuwa akituma misafara kwenda barani Afrika kukamata watumwa na kuwaleta kisiwani kufanya kazi katika nyanja za karafuu au kupakiwa ng'ambo. Kila mwaka katika utawala wa Said bin Sultan na mrithi wake, Sayyid Majid bin Said Al-Busaid, takribani watumwa elfu hamsini waliuzwa katika soko Jijini Zanzibar. Bennett katika kitabu chake, *Historia ya Jimbo la Waarabu la Zanzibar,* anasema, "Katika mwisho wa mwongo wa 1850 takribani theluthi mbili ya wakazi elfu mia tatu wa kisiwa walikuwa watumwa"[3]. Kweli watumwa walikuwa wengi kisiwani na siamini mbona hakukuwa na vita baina ya Waarabu na watumwa wao.

[3] Tafsiri kutoka Bennett, ukurasa 28.

Hatimaye katika utawala wa Sayyid Barghash bin Said Al-Busa (1870-1888), pamoja na bidii za watawa kutoka Ulaya, biashara ya watumwa iliachwa katika mwaka wa 1873. Uamuzi huu ulikuja baada ya Jiji la Zanzibar kuchukuliwa na Uingereza katika 1862 ili kuwa mahamio ya Uingereza[4].

Katika kipidi cha ukoloni wa Uingereza, katika Mji wa Mawe madaraja ya reli na ya barabara yalijengwa. Mji uliendelea kuongezeka idadi ya wakazi na majengo hadi mwaka wa 1963, Unguja ilipopata uhuru. Abeid Amani Karume alikuwa rais wa kwanza wa Unguja na katika mwaka wa 1964 aliamua kuunganisha kisiwa na Tanganyika ya bara kuunda nchi ya Tanzania ya leo. Tangu wakati wa uhuru, hakuna majengo mengi ambayo yamejengwa Jijini Zanzibar lakini idadi ya watu haijasimama kuongezeka. Kwa hivyo, Jiji la Zanzibar ya leo ni mahali pa misongamano na uchafu. Lakini, hivi karibuni, watu wameanza kutambua kwamba Mji wa Mawe una thamani nyingi na kuanza kulinda hisotria ya mji wao. Ukweli ni kwamba watalii wengi wanataka kutembelea Mji wa Mawe kwa sababu ya historia yake na wanaleta pesa za kigeni.

Vivutio vya Jiji la Zanzibar

Ukitembelea Jiji la Zanzibar hutakuwa na uchovu kwa sababu kuna vitu vingi vya kufanya na sehemu nyingi unazoweza kuzitembelea. Kivutio kikubwa zaidi ni Mji wa Mawe ambapo unaweza kwenda kujifunza kuhusu historia ya kisiwa hiki maridadi.

Katika Mji wa Mawe, kuna majengo mengi ya kihistoria na mtu ambaye anayatembelea afadhali afurahi kabisa. *Beit el Ajaib* (maana yake katika Kiingereza ni *‘House of Wonders’)* ndilo jengo lililo na umaaraufu zaidi katika Mji wa Mawe. Jengo hili lilikuwa kasri ya sultani na lilijengwa na Sayyid Barghash bin Said Al-Busa katika mwaka wa 1883. Linapakana na ufuko

[4] Tarehe zinatoka Fitzpatrick, ukurasa 143.

na unapata mandhari maridadi ya bahari kutoka ghorofa zake. Leo jengo hili ni jengo la kumbukumbu na kila siku, linafurahisha wageni wengi.

Ukienda kaskazini kutoka *Beit el Ajaib* utafika *Ngome Kongwe,* ambayo ilijengwa na Waarabu mnamo mwaka wa 1700 ili walinde mji wao mpya. Hivi karibuni, ngome hii imefanywa mpya ndani na leo ni mahali pa kituo cha Utamaduni wa Unguja. Kuna jumba la michezo ya kuigiza ambapo watalii wanafurahishwa na mambo tofauti kama muziki, dansi ya jadi na kadhalika. Pia, hapo *Ngome Kongwe* kuna maduka ambayo yanauza zawadi za kumbukumbu.

Majengo mengine ambayo labda mtu atataka kutembelea yanajumuisha *Nyumba ya Livingstone na Zahanati ya Zamani. Nyumba ya Livingstone* ilijengwa mnamo mwaka wa 1860. Ilikuwa makazi ya watawa na wavumbuzi kutoka Ulaya kabla ya kuondoka kwenda bara la Afrika. Mvumbuzi maarufu, David Livingstone, alikaa hapo kabla ya safari yake ya mwisho katika mwaka wa 1866. *Dispensari ya Zamani* iko barabarani Mizingani, karibu na bandari na ilijengwa na mchuuzi Mhindi mnamo mwaka wa 1900. Leo, utapata maduka mbalimbali pale.

Kwa sababu Jiji la Zanzibar linapakana na Bahari Hindi, kuna vitu vingi vya kukufurahisha. Unaweza kukodisha mashua kusafiri baharini kuvua samaki au kutembelea visiwa vidogo karibu na Unguja. Aidha, kuna fuko nyingi maridadi ambapo unaweza kutembea au kupumzika chini ya jua. Kama hupendi bahari au ufuko, lakini wewe ni mwanamichezo, kwenda katika uwanja wa Mnazi Mmoja ambapo kila Jumapili wananchi wanajumuika kucheza kandanda.

Mahali pa Kukaa, Kula na Kwenda nje jioni.

Ukitembelea Jiji la Zanzibar na uwe na pesa nyingi za kutumia, mahali safi pa kukaa ni *Zanzibar Serena Inn.* Kukaa *Serena* kunachukua dola mia moja themanini na tano kwa mtu mmoja, au dola mia mbili na themanini kwa watu wawili, kwa usiku mmoja. Lakini ukitaka mahali pa bei rahisi, ni lazima ukae katika *Pyramid Hotel* ambapo utalipa dola kumi kwa mtu mmoja kwa usiku mmoja. Vyumba vya Pyramid havipendezi sana lakini ni safi.

Kuna mahali pengi ambapo utaweza kupata chakula kitamu. Afadhali uende *Forodhani Gradens* kuonja chakula cha mitaa. Wapishi wanachoma chakula mbalimbali cha bahari, kwa mfano kaa, tewa na ngisi, katika vibanda vya vyakula, na hapo utashiba kabisa kwa bei rahisi. Hoteli nyingine ambayo ni maarufu kwa sababu ya chakula chake ni *Luna Mare.* Hapo wanauza chakula cha Uhindi na Uchina na kweli utafurahi ukionja chakula chao.

Ikiwa ni usiku, baada ya kula katika hoteli nzuri, ukitaka kwenda nje kucheza ngoma au labda kunywa pombe na mwenzako, jaribu *Baa ya Livingstone* au *The Garage Club*. Hapo, *Baa ya Livingstone,* utaweza kununua bia za Kenya, Tanzania, Afrika Kusini na Ujerumani. Afadhali ujaribu bia ya Tanzania inayoitwa *Safari* ili uonje utamaduni wenyewe wa Unguja!

Jijini Zanzibar utakapotafuta vitu ambavyo vitakustarehesha, ukweli ni kuwa hutakuwa na matatizo. Aidha, wananchi wa Jiji la Zanzibar ni wakarimu na wacheshi. Wanapenda maisha sana, na utafurahi kukutana nao. Ukisafiri Jiji la Zanzibar, itakuwa safari bora zaidi katika maisha yako!

Marejeleo

Bennett , Norman R. *A History of the Arab State of Zanzibar*. Holborn, London: Cambridge University Printing House, 1978

Fitzpatrick, Mary. *Tanzania, Zanzibar and Pemba.* Victoria, Australia: Lonely planet Publications Pty Ltd, 1999.

http://www.tanzania.go.tz/census/

http://www.africatravelresource.com/africa/E/zanzibar/accommodation/00.htm#

http://home.globalfrontiers.com/Zanzibar/swahili_home_page.htm